

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

PARLIAMENT OF TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI NA TANO

23 APRILI, 2018



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI NA TANO – TAREHE 23 APRILI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.



MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE  
YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya

Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

##### **115. MHESHIMIWA AMINA SALEH MOLLEL (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Utekaji nyara na mauaji ya Watu wenyе Ulemavu wa Ngozi (Albino) vilikithiri kwenye miaka ya 2000 hali iliyopelekea Serikali kuanzisha kambi maalum kwa ajili ya usalama wao:-

- (a) Je, Serikali imeanzisha kambi ngapi mpaka sasa na ni katika Mikoa na Wilaya zipo;
- (b) Je, ni Watu wangapi wenyе Ulemavu wa Ngozi wanaoishi katika makambi hayo.

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **116. MHESHIMIWA ZACHARIA PAUL ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Mbulu

inakabiliwa na upungufu mkubwa wa Watumishi; upungufu huo wa Watumishi umeathiri utoaji wa huduma kwa Hospitali hiyo na Vituo vya Afya vya Tlawi na Daudi:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza Watumishi katika Hospitali hiyo;
- (b) Serikali inatekeleza mpango wa upanuzi wa Vituo vya Afya zaidi ya 200 Nchini, Je, Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na changamoto za Watumishi, fedha na vitendea kazi.

#### **117. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni eneo gani limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kubangua Korosho katika Manispaa ya Mtwara Mikindani.

#### **118. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Jimbo la Segerea ni moja kati

ya Majimbo ya Dar es Salaam ambalo wakazi wake wengi wana kipato cha chini na sababu kubwa ikiwa ni ubovu wa miundombinu ya barabara hasa madaraja na mitaro hivyo kusababisha mafuriko ya mara kwa mara:- Je, ni lini Serikali itajenga madaraja ya Tabata Kisiwani na Kisukuru sambamba na kujenga mitaro ili kupunguza adha ya mafuriko katika Kata za Jimbo hili.

#### **WIZARA YA NISHATI:**

##### **119. MHESHIMIWA JAMAL KASSIM ALI (MAGOMENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulifanya Shirika la Umeme (TANESCO) lijiendeshe kwa faida.

##### **120. MHESHIMIWA SILVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Mradi wa Umeme wa 400KV kutoka Kinyerezi hadi Arusha umepitia maeneo mengi ya nchi yetu ikiwa ni pamoja na Jimbo la Kibaha Mjini, uthamini wa mali za waathirika ulishafanyika toka 2015:-

Je, Serikali itawalipa lini Wananchi hawa.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:**

**121. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL  
ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Mpaka sasa inadaiwa kuwa hakuna dawa sahihi za kutibu ugonjwa wa kisukari:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti kuhusu dawa za kisukari.

**122. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLA SALIM  
(MTAMBILE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Imebainika kuwa ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB) umeendelea kuathiri Jamii ya Watanzania:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na ongezeko la Wagonjwa wa TB.



## **WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

### **123. MHESHIMIWA ZUBEDA HASSAN SAKURU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya muda mrefu katika kuimarisha ushiriki wenyewe tija kwa Tanzania katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa.

## **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

### **124. MHESHIMIWA MARIA NDILLA KANGOYE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:- Kumekuwa na changamoto nyingi katika uvubi wa Ziwa Victoria unaosababisha malalamiko mengi kutoka kwa wadau wa uvubi:-

Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha inamaliza malalamiko hayo.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

DODOMA  
23 APRILI, 2018

S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE



BUNGE LA TANZANIA